MWITO PROG 1124 KISWAHILI SCRIPT

SCRIPTURE:ROMANS 7:23-25

TRANSWORLD RADIO

INTRO:

Kwa mara nyingine tena idhaa hii inakuletea kipindi cha Mwito.Ninaamkni kuwa hujambo msikilizaji wangu na kwamba u tayari tena kujumuika name kwa hiki kipindi cha Mwito.Makala ya leo ni nambari 1124.Ninakupatia nambari hiyo ili uweze kujua ni kipindi gani ambacho labda ulikuwa na swali nacho au hukukifahamu vizuri.Kama ilivyo ada nakufahamisha kuwa kipindi hiki kimefadhiliwa na huduma ya Kimataifa ya Macedonian Call chake mchungaji Harold Williams.Katika muda wa dakika 15 zijazo tutasoma pamoja maandiko kutoka kitabu cha Warumi na kufafanua aya kwa ya na sura kwa sura.Lengo la kipindi hiki ni kukushirikisha katika mbnu za uenezaji wa neno la Mungu kwa njia zoteIkiwa ungependa kupokea Biblia baki nami kwa muda huo kwa kuwa jinsi gani unavyoweza kujipatia agano jipya la Biblia.

Warumi sura ya 7 na aya za 22-23 zinasema hivi***…Kwa maana naifurahia sheria iliyo katika viungo vyangu. Mungu kwa utu wa ndani.Lakini katika viungo vyangu naona sheria iliyo mbali,inanipiga vita na ile sheria ya akili zangu,na kunifanya mateka wa ile sheria ya dhambi iliyo katika viungo vyangu.***

Hiyo ndiyo sehemu tulioisoma kwenye kipindi kilichopita.Na kwenye kipindi hiki tutakamilisha sura ya 7 ya kitabu hiki cha Warumi.Naomba ufungue nami kutoka aya ya 23 hadi 25- ***Kwa maana naifurahia sheria iliyo katika viungo vyangu. Mungu kwa utu wa ndani.Lakini katika viungo vyangu naona sheria iliyo mbali,inanipiga vita na ile sheria ya akili zangu,na kunifanya mateka wa ile sheria ya dhambi iliyo katika viungo vyangu.***

Hao ndio tulimalizia somo lililopita.Tulichunguza ukinzani ulioko ksati ya nafsi ha kale na ile mpya yaani utu upya.Mkanganyo huu umeifanya sura ya 7 ya warui kutoeleweka kwa watu wengi.Ukweli ni kwamba shetani angependa kukubwaga chini ikiwa wewe ni mwaminio.Hilo ndilo lengo lake.Angependa uhisi kwamba kwa kweli hujaokoka kwa luwa unashindwa kuishi

maisha ya ushindi.Na kama angetaka kutuma silaha hiyo kukutatiza kwamba hujokoka,japo wewe una hsakika umeokoka,atatumia kisababu hicho kuondoa ushawiki ambao ungetumia kuwaambia wengine kuhusu neema na Mungu na nguvu zilizo katika neno lake.Hilo ha.itamfurahisha Mungu kwa kuwa utazidi kuishi maisha ya kushindwa.Hilo nalo litakukosesha thawabu mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo.

Lakini kama umepokea Kristo kuwa mwokozi wako ulifika mahali ambapo ulingámua kwamba huwezi bila mwokozi Yesu.Ulifahamikiwa kuwa ulikuwa kwenye njia kuu ielekeayo jehenamu.Lakini kwa wakati muafaka na kwa neema na rehema yake ulipata kulisikia neno na ukafanya uamuzi wa kurejesha uhusiano na Mungu muumba wako kupitia njia ya wokovu kwa damu ya Yesu kristo iliomwagika pale kalvari.Lakini naona unajuliza ikiwa ni hivyo mbona bado ninatatizika katika maisha yangu ya ukristo.Ukwe.i ni kwamba ukisoma mara kadhaa sura za 6 na 7 za Warumi kwa pamoja,utafahamikiwa kuwa maisha ya mkristo ni maisha ya mapambano.Mapambano kati ya utu wa kale na ule mpya tunopokea tunapomkubali

kristo kuwa mwikozi wetu.Mpendwa ikiwa u eokoka ni hivyo.Na Yesu alikuokoa kikamilifu ili utumike katika kazi yake ya kueneza injili.Hakuna msitari usemao kuwa tuliokokolewa kwa muda fulani au kipindi fulani.Ama umeokoka au hujaokoka.Hakuna jingine hapo katikati.Ikiwa hujaokoka basi kipindi hiki ndicho sababu ya kukuletea ujumbe wa wokovu..injili ya wokovu.Ikiwa hujaokoka huu ni wakati mzuri wa kupiga magoti na kumwomba Yesu akuokoe kwa sababu anakupenda na anakujali.Kitabu cha mhubiri kinatuambia kuwa lolote afanyalo Mungu,hulifanya kikamilifu.Hakuna la uongezea wala kuondoa kwa neno lake na Mungu anatukuzwa kwa hilo.Sheria ya dhambi na kifo imetumiwa na ibilisi kutufunga sana.Lakini kuna sheri ya Mungu ambayo kwayo tunapata ushindi.Naam mpendwa ikiwa vita hivyo ndani yako ni kama vile vya pili vya dunia ,basi bado hujakomaa kiroho.Ushindi kamili kwako na kwangu mpendwa utapatikana tu tutakaomshinda ibilisi na mbinu zake zote na kudumu katika kumfanyia kazi.Bila shaka kutakuwa na matatizo na pingamizi,lakini tumehakikishiwa ushindi katika Kristo.Ukomavu

katika neno la Mungu utatuwezesha kushinda hizo pingamii za muovu.Sikiza jinsi aya za 24 na 25 zinavyosema….***Ole wangu maskini mimi.Ni nani ataniokoa na mwili huu wa mauti? Namshkuru Mungu kwa Yesu Bwana wetu.Basi kama ni hivyo mimi mwenyewe kwa akili zangu naitumikia sheria ya Mungu,bali kwa mwili wangu sheria ya dhambi.***

Labda wengine wenu mnaweza kuambiwa kuwa watu fulani tangu kuokoka hawajaona ugumu wowote wala kutenda maudhi mbele za MUngu.Yaani wao wanapuruka tu kwa mabawa wala tatizo lolote hawana.Hiyo si kweli.

Kumbuka tena maneno ya mtume Paulo… ***Ole wangu maskini mimi.Ni nani ataniokoa na mwili huu wa mauti? Namshkuru Mungu kwa Yesu Bwana wetu.***Sasa mpendwa ukweli ndio huo kwamba Kristo Yesu atamwsokoa mwaminio kutokana na mwili wa Mauti.Wale walio na shsauku ya kumshinda ibilisi na kazi zake.Kwamba…. ***mimi mwenyewe kwa akili zangu naitumikia sheria ya Mungu,bali kwa mwili wangu sheria ya dhambi.***

Tunakumbushwa tena hapo kuhusu vita au mvutano kati ya utu wa kale n ule upya wa Kristo.Roho ya mwaminio daima

ingepednda kumwandamia Kristo,lakini mwili hukinzana na azma hiyo.Namalizia kwa kuuliza ikiwa una utu upya wa Kristo ndano yako.Yaani umeokoka au bado.Fursa ni hii.Tubu dhambi zako na umwamini Kristo kwamba yuaweza kulinda kilichoekwa amana kwake Bwana.Naomba nikomee hapa.

Tubu dhambi zako na umkubalie Yesu kuongoza maisha yako.Ukishatubu,tafahadhali mwende mwongofu yeyote anayeamini injili ya wokovu ambaye atakuelekeza kwa kanisa litakalokusaidia kukua kiroho.IKiwa unahudhuria kanisa linaloamini wokovu.Aidha mwende mchungaji wako na umweleze hatua ambayo umechukua naye atakusaidia. unaweza pia kuniandikia au unipigie simu na nitakuelekeza cha kufanya ili uweze kuhifadhi wokovu wako.Na kufikia hapa ndipo natia tamati kipindi hiki cha Mwito nambari 1124.Naomba tukutane katika makala yajayoo.Mwalike rafiki yako ili mkidikilize pamoja kipindi hiki na mtutumie maoni yenu kuhusu jinsi h kukiboresha. Tunakukaribisha ututembelee kwenye studio zetu za TWR Kamburu Drive,off Ngong Road, baada ya jumba la TOP PLAZA.Anwani yangu ikiwa utaniandikia barua

ni-:Kwa mtayarishi,Mwito,S.L.P.21514-00505 Nairobi.Nitumie arafa yako kwa nambari hii -0721 970 520. Au 020 2679842 Waweza pia kuwasiliana nami kwa njia ya barua pepe ifwatavyo-barua@twr.co.ke.Na basi kufikia hapo sina budi kulikunja jamvi langu kwa leo ninapokutakia baraka sufufu kutoka kwake Mungu wetu mtukuka.Juma lijalo tutaingia aya ya kwanza ya sura ya 8 ya kitabu cha Warumi.Ni mimi ndugu Charles Otunga ninayekuaga nikikutakia mibaraka na neema tele zake zake Mungu.Bwana akubariki na udumu katika neema yake.Kwaheri.